



## ***Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo***

### **1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MACHI, 2023 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 MACHI, 2023.**

#### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MACHI, 2023.**

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliimarika kidogo wakati ile iliyopo katika kizio cha Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) haikua na mabadiliko. Hali hii iliendelea kuchochea uwepo wa Ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusalia katika baadhi ya maeneo ya magharibi mwa nchi na ukanda wa ziwa Victoria. Joto la bahari katika eneo kubwa la bahari ya Hindi lilikua la wastani hadi chini kidogo ya wastani na hivyo kutokua na mchango katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka katika bahari ya Hindi kuelekea katika maeneo ya pwani ya nchi. Aidha, kuimarika kwa mfumo wa wimbi anga (Madden Julian Oscillation) kulichangia uwepo wa mvua na ngurumo katika baadhi ya maeneo nchini.

#### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MACHI, 2023.**

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi hususani katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria, Magharibi, Kusini na Nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya ukanda wa pwani. Hata hivyo, maeneo mengine ya nchi kwa ujumla yalipata mvua nyepesi hadi mvua za wastani.

### **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-31 MACHI, 2023.**

#### **2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 MACHI, 2023.**

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo katika kizio cha Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kudhoofika kidogo. Hali hii inatarajiwa kuusukuma Ukanda mvua

(ITCZ) kuelekea Kaskazini hususani katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu kidogo hususani katika maeneo ya Kaskazini mwa Madagascar na inatarajiwa kusababisha uwepo wa migandamizo midogo ya hewa. Hali kadhalika, mfumo wa wimbi anga (MJO) unatarajiwa kuendelea kuimarika na hivyo kuendelea kusababisha vipindi vya mvua na ngurumo kwa baadhi ya maeneo.

## **2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 MACHI, 2023.**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa kwa baadhi ya maeneo.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo zinatarajiwa.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Imetolewa na;

## **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**